

**TAARIFA KWA UMMA KUHUSU BEI KIKOMO ZA MAFUTA AINA YA PETROLI KUENZIA JUMATANO, TAREHE 7 FEBRUARI 2018**

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), inatangaza bei kikomo za bidhaa za mafuta ya petroli hapa nchini. Bei hizi zitaanza kutumika kuanzia **Jumatano, Tarehe 7 Februari 2018**. Pamoja na kutambua bei kikomo za bidhaa mbalimbali za petroli nchi nzima, ni muhimu kuzingatia yafuatayo:-

- (a) Bei za jumla na rejareja kwa mafuta ya aina zote (Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa) yaliyoingizwa nchini kupitia bandari ya Dar es Salaam, zimeongezeka ikilinganishwa na toleo lililopita la tarehe 3 Januari 2018. Kwa mwezi Februari 2018, bei za rejareja za Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa zimeongezeka kwa Shilingi 59/lita (sawa na asilimia 2.70), Shilingi 46/lita (sawa na asilimia 2.30) na Shilingi 24/lita (sawa na asilimia 1.17) sawia. Vilevile, kwa kulinganisha na toleo la mwezi uliopita, bei za jumla za Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa zimeongezeka kwa Shilingi 58.57/lita (sawa na asilimia 2.85), Shilingi 46.48/lita (sawa na asilimia 2.44) na Shilingi 23.75/lita (sawa na asilimia 1.24) sawia. Ongezeko la bei za mafuta ya Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa limetokana na ongezeko la bei za mafuta hayo katika soko la dunia.
- (b) Bei za jumla na rejareja kwa mafuta ya Petroli na Dizeli yaliyoingizwa nchini kupitia bandari ya Tanga nazo zimeongezeka ikilinganishwa na toleo lililopita la tarehe 3 Januari 2018. Bei za Mafuta ya Taa hazijabadilika kwa sababu hakuna Mafuta ya Taa yaliyoingizwa nchini kupitia bandari ya Tanga katika mwezi wa January 2018. Katika toleo hili, bei za rejareja za Petroli na Dizeli kwa **Mikoa ya Kaskazini** zimeongezeka kwa Shilingi 15/lita (sawa na asilimia 0.70) na Shilingi 47/lita (sawa na asilimia 2.29), sawia. Aidha, kwa kulinganisha na toleo la mwezi uliopita, bei za jumla za Petroli na Dizeli zimeongezeka kwa Shilingi 15.36/lita (sawa na asilimia 0.73) na Shilingi 47.18/lita (sawa na asilimia 2.42). Ongezeko la bei za mafuta ya Petroli na Dizeli katika mkoa wa Tanga linatokana na mabadiliko ya bei za mafuta hayo katika soko la dunia na kuongezeka kwa gharama za usafirishaji (*BPS premiums*).
- (c) Ifahamike kwamba, sehemu kubwa ya shehena za mafuta yaliyopokelewa katika bandari ya Dar es Salaam ni zile zenye bei za soko la dunia za mwezi Novemba 2017 wakati shehena iliyopokelewa katika bandari ya Tanga ni ya bei za soko la dunia za mwezi Desemba 2017. Bei za mafuta katika soko la dunia kwa mwezi Novemba 2017 ziko juu kwa zaidi ya asilimia 6 ikilinganishwa na bei za mwezi Oktoba 2017 wakati bei za mwezi Desemba zina mabadiliko tofauti, ambapo bei za Petroli zimepungua kwa asilimia 0.2 na bei za Dizeli na Mafuta ya Taa zimeongezeka kwa asilimia 2.7 na asilimia 1.9, sawia.
- (d) Mamlaka inapenda kuukumbusha umma kwamba bei kikomo za mafuta kwa eneo husika, zinapatikana pia kupitia simu za mkononi kwa kupiga namba **\*152\*00#** na kisha kufuata maelekezo. Huduma hii ni bure na inapatikana kupitia mitandao yote ya simu za mkononi hapa nchini.
- (e) Kwa mujibu wa Sheria ya Mafuta ya mwaka 2015, bei za bidhaa za mafuta ya petroli zitaendelea kupangwa na soko. EWURA itaendelea kuhamasisha ushindani kwa kutoa taarifa za bei kikomo za

bidhaa za mafuta. Taarifa hizi zina lengo la kuwasaidia wadau kufanya maamuzi stahiki kuhusu manunuzi ya bidhaa za mafuta.

- (f) **Kampuni za mafuta ziko huru kuuza bidhaa za mafuta ya petroli kwa bei ya ushindani mradi tu bei hizo zisivuke bei kikomo (*price cap*) kama ilivyokokotolewa na kanuni (*formula*) iliyopitishwa na EWURA na ambayo ilichapishwa katika **Gazeti la Serikali Na. 216/2017 la mwezi Mei 2017.****
- (g) Vituo vyote vya mafuta vinatakiwa kuchapisha bei za bidhaa za mafuta katika mabango yanayoonekana bayana na yakionesha bei ya mafuta, punguzo, vivutio vya biashara au promosheni zinazotolewa na kituo husika. Pale ambapo inawezekana kuchagua, wateja wanashauriwa kununua bidhaa za mafuta katika vituo vinavyouza mafuta kwa bei nafuu zaidi ili kushamirisha ushindani. **Ni kosa kuuza mafuta bila kuweka mabango ya bei inayoonekana vizuri kwa wateja. Adhabu kali itatolewa kwa kituo husika kwa kutotekeleza matakwa ya kisheria kwa mujibu wa kanuni husika.**
- (h) Wauzaji wa mafuta ya petroli wanatakiwa kutoa risiti za mauzo kutoka kwenye mashine za EFPP (*Electronic Fiscal Pump Printers*) na Wanunuzi wahakikishe wanapata stakabadhi hizo za malipo zinazoonyesha jina la kituo, tarehe, aina ya mafuta yaliyonunuliwa na bei kwa lita. Stakabadhi hizo za malipo zitatumika kama kidhibiti kwa wanunuzi wa mafuta endapo kutajitokeza malalamiko ya aidha kuuziwa mafuta kwa bei ya juu kuliko bei kikomo au kuuziwa mafuta yasiyo na kiwango cha ubora kinachofaa, na pia, risiti hizo zitasaidia kurahishisha ukusanyaji wa kodi za Serikali zitokanazo na mafuta ya petroli.

#### A: BEI ZA REJAREJA

Mji	Bei Kikomo		
	Petroli (Shs/Lita)	Dizeli (Shs/Lita)	Mafuta Ya Taa (Shs/Lita)
<b>Dar es Salaam</b>	<b>2,226</b>	<b>2,065</b>	<b>2,055</b>
<b>Arusha</b>	<b>2,278</b>	<b>2,163</b>	<b>1,995</b>
Arumeru (Usa West)	2,278	2,163	1,995
Karatu	2,297	2,181	2,013
Monduli	2,284	2,168	2,000
Monduli-Makuyuni	2,288	2,173	2,005
Ngorongoro (Loliondo)	2,363	2,247	2,079
<b>Kibaha</b>	<b>2,231</b>	<b>2,069</b>	<b>2,059</b>
Bagamoyo	2,237	2,076	2,066
Kisarawe	2,233	2,072	2,062
Mkuranga	2,236	2,074	2,064
Rufiji	2,254	2,092	2,082
<b>Dodoma</b>	<b>2,285</b>	<b>2,123</b>	<b>2,113</b>
Bahi	2,292	2,131	2,121
Chemba	2,311	2,150	2,140
Kondoa	2,317	2,156	2,146
Kongwa	2,282	2,121	2,111
Mpwapwa	2,286	2,124	2,115
<b>Iringa</b>	<b>2,290</b>	<b>2,129</b>	<b>2,119</b>
Kilolo	2,294	2,133	2,123

Mufindi (Mafinga)	2,300	2,139	2,129
<b>Njombe</b>	<b>2,318</b>	<b>2,157</b>	<b>2,147</b>
Njombe (Kidegembye)	2,339	2,177	2,168
Ludewa	2,356	2,195	2,185
Makete	2,349	2,188	2,178
Wanging'ombe (Igwachanya)	2,316	2,155	2,145
<b>Bukoba</b>	<b>2,441</b>	<b>2,280</b>	<b>2,270</b>
Biharamulo	2,415	2,254	2,244
Karagwe (Kayanga)	2,457	2,296	2,286
Kyerwa (Ruberwa)	2,463	2,302	2,292
Muleba	2,441	2,280	2,270
Ngara	2,406	2,245	2,235
Misenyi	2,449	2,288	2,278
<b>Geita</b>	<b>2,391</b>	<b>2,230</b>	<b>2,220</b>
Bukombe	2,380	2,219	2,209
Chato	2,412	2,251	2,241
Mbogwe	2,429	2,268	2,258
Nyang'hwale	2,406	2,245	2,235
<b>Kigoma</b>	<b>2,457</b>	<b>2,295</b>	<b>2,286</b>
Uvinza (Lugufu)	2,469	2,308	2,298
Buhigwe	2,446	2,285	2,275
Kakonko	2,414	2,253	2,243
Kasulu	2,443	2,282	2,272
Kibondo	2,421	2,260	2,250
<b>Moshi</b>	<b>2,268</b>	<b>2,152</b>	<b>1,984</b>
Hai (Bomang'ombe)	2,271	2,156	1,988
Mwanga	2,261	2,145	1,977
Rombo (Mkuu)	2,285	2,169	2,001
Same	2,254	2,139	1,971
Siha (Sanya Juu)	2,274	2,159	1,991
<b>Lindi</b>	<b>2,285</b>	<b>2,123</b>	<b>2,114</b>
Lindi-Mtama	2,303	2,141	2,132
Kilwa Masoko	2,260	2,098	2,089
Liwale	2,306	2,144	2,134
Nachingwea	2,314	2,153	2,143
Ruangwa	2,316	2,154	2,144
<b>Babati</b>	<b>2,312</b>	<b>2,197</b>	<b>2,029</b>
Hanang (Katesh)	2,323	2,207	2,039
Kiteto (Kibaya)	2,328	2,212	2,044
Mbulu	2,325	2,209	2,041
Simanjiro (Orkasumet)	2,344	2,229	2,061
<b>Musoma</b>	<b>2,404</b>	<b>2,243</b>	<b>2,233</b>
Musoma Vijijini (Busekela)	2,445	2,283	2,274
Rorya (Ingirijuu)	2,413	2,252	2,242
Rorya (Shirati)	2,448	2,286	2,276
Bunda	2,395	2,234	2,224
Butiama	2,401	2,240	2,230
Serengeti (Mugumu)	2,450	2,288	2,278

Tarime	2,415	2,254	2,244
Tarime (Kewanja/Nyamongo)	2,420	2,258	2,248
<b>Mbeya</b>	<b>2,333</b>	<b>2,171</b>	<b>2,162</b>
Chunya	2,342	2,181	2,171
Chunya (Makongolosi)	2,357	2,195	2,185
Ileje	2,346	2,185	2,175
Kyela	2,349	2,187	2,177
Mbarali (Rujewa)	2,317	2,156	2,146
Mbozi (Vwawa)	2,342	2,181	2,171
Momba (Chitete)	2,351	2,190	2,180
Rungwe (Tukuyu)	2,342	2,180	2,171
<b>Morogoro</b>	<b>2,251</b>	<b>2,090</b>	<b>2,080</b>
Mikumi	2,267	2,105	2,095
Kilombero (Ifakara)	2,289	2,127	2,117
Kilombero (Mlimba)	2,311	2,150	2,140
Kilombero (Mngeta)	2,300	2,139	2,129
Ulanga (Mahenge)	2,299	2,138	2,128
Malinyi	2,310	2,148	2,138
Kilosa	2,269	2,108	2,098
Gairo	2,269	2,108	2,098
Mvomero (Wami Sokoine)	2,261	2,100	2,090
Turiani	2,276	2,115	2,105
<b>Mtwara</b>	<b>2,298</b>	<b>2,137</b>	<b>2,127</b>
Nanyumbu (Mangaka)	2,347	2,186	2,176
Masasi	2,324	2,162	2,153
Newala	2,330	2,169	2,159
Tandahimba	2,323	2,162	2,152
<b>Mwanza</b>	<b>2,376</b>	<b>2,214</b>	<b>2,205</b>
Kwimba	2,412	2,250	2,241
Magu	2,384	2,222	2,213
Misungwi	2,381	2,220	2,210
Sengerema	2,408	2,247	2,237
Ukerewe	2,435	2,274	2,264
<b>Sumbawanga</b>	<b>2,398</b>	<b>2,237</b>	<b>2,227</b>
Kalambo (Matai)	2,406	2,244	2,234
Nkasi (Namanye)	2,412	2,251	2,241
Katavi (Mpanda)	2,433	2,272	2,262
Mlele (Inyonga)	2,412	2,250	2,241
<b>Songea</b>	<b>2,349</b>	<b>2,188</b>	<b>2,178</b>
Mbinga	2,383	2,221	2,211
Namtumbo	2,378	2,217	2,207
Nyasa (Mbamba Bay)	2,385	2,224	2,214
Tunduru	2,408	2,247	2,237
<b>Shinyanga</b>	<b>2,355</b>	<b>2,193</b>	<b>2,183</b>
Kahama	2,368	2,207	2,197
Kishapu	2,383	2,222	2,212
Simiyu (Bariadi)	2,396	2,235	2,225
Busega (Nyashimo)	2,389	2,228	2,218

Itilima (Lagangabilili)	2,399	2,238	2,228
Maswa	2,387	2,226	2,216
Meatu (Mwanhuzi)	2,394	2,233	2,223
<b>Singida</b>	<b>2,316</b>	<b>2,155</b>	<b>2,145</b>
Iramba	2,329	2,167	2,157
Manyoni	2,301	2,140	2,130
Ikungi	2,312	2,151	2,141
Mkalama (Nduguti)	2,341	2,180	2,170
<b>Tabora</b>	<b>2,380</b>	<b>2,219</b>	<b>2,209</b>
Igunga	2,334	2,173	2,163
Kaliua	2,398	2,237	2,227
Ulyankulu	2,392	2,231	2,221
Nzega	2,344	2,183	2,173
Sikonge	2,392	2,230	2,220
Urambo	2,393	2,232	2,222
<b>Tanga</b>	<b>2,222</b>	<b>2,106</b>	<b>1,938</b>
Handeni	2,242	2,127	1,959
Kilindi	2,257	2,142	1,974
Korogwe	2,234	2,118	1,950
Lushoto	2,243	2,128	1,960
Mkinga (Maramba)	2,229	2,113	1,945
Muheza	2,227	2,111	1,943
Pangani	2,228	2,113	1,945

**B: BEI ZA JUMLA**

<b>Bei za Jumla – DSM</b>	<b>Petroli (Shs/Lita)</b>	<b>Dizeli (Shs/Lita)</b>	<b>Mafuta ya Taa (Shs/Lita)</b>
<b>Bei Kikomo</b>	<b>2,114.99</b>	<b>1,953.60</b>	<b>1,943.75</b>

<b>Bei za Jumla – TANGA</b>	<b>Petroli (Shs/Lita)</b>	<b>Dizeli (Shs/Lita)</b>	<b>Mafuta ya Taa (Shs/Lita)</b>
<b>Bei Kikomo</b>	<b>2,110.83</b>	<b>1,995.12</b>	<b>1,827.17</b>

**Nzinyangwa Mchany**  
**KAIMU MKURUGENZI MKUU**  
**EWURA**